



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI



(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

SIMU NA.0737235630
Email- ded.itigidc@singida.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi
01 Barabara ya Halmashauri
S.L.P 70,
43483 ITIGI - SINGIDA

Kumb.Na. HW/ITG/S.1/22 VOL.III/75

27 Julai, 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Itigi imepokea idhini ya utekelezaji wa Ajira Mpya kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kupitia barua yenye Kumb.Na.FA.170/336/01'B'55 cha tarehe 27 Juni, 2022 Kutoka kwa Katibu Mkuu (Utumishi), Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi anawatangazia wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi ifuatayo:-

1. MTUNZA KUMBUKUMBU DARAJA LA II – (NAFASI 3)

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI)
- Awe na astashahada/cheti NTA Level 5 cha mafunzo ya utunzaji kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya na Masjala.

KAZI NA MAJUKUMU YA MTUNZA KUMBUKUMBU:-

- i. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/majalada yanayohitajiwa na wasomaji.
- ii. Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka za Ofisi.
- iii. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (Classification and Boxing) kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.
- iv. Kuweka, kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki (file racks/cabinet) katika masjala /vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.
- v. Kuweka kumbukumbu (barua , nyaraka n.k) katika majalada.
- vi. Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/nyaraka kutoka Taasisi za Serikali; na
- vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

MSHAHARA

- Kwa kuzingatia Ngazi ya Mishahara ya Serikali, yaani TGS B kwa Mwezi


2. MASHARTI YA JUMLA YA MWOMBAJI KAZI

- Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka kumi na nane (18) na usiozidi miaka arobaini na tano (45)
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- Waombaji waambatanishe na maelezo yao binafsi (C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina matatu ya wadhamini (Referees) wa kuaminika.
- Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha (IV na VI), na picha mbili (2) za rangi (passportsize) za hivi karibuni katika barua ya maombi. Pia nakala zote za vyeti zithibitishwe na Mwanasheria au wakili yeyote aliyesajilwa na kuthibitishwa.
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE
- **“Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati ya Matokeo ya Kidato cha Nne na Sita (FORM IV and FORM VI RESULT SLIPS) HAVITAKUBALIWA**
- Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria
- Waombaji wa kazi ambao tayari ni waajiriwa katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyopo katika waraka Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30/11/2020.
- Awe hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai
- Waombaji wote wawe na kitambulisho cha NIDA au namba ya kitambulisho.
- Waombaji watakaokidhi sifa ndio watakaitwa katika usaili
- Maombi yatumwe kwa njia ya Posta
- Barua ya maombi iandikwe kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza
- Waombaji wenye mahitaji maalum (special needs/disability) wanatakiwa kuainisha kwenye maombi.
- Waombaji ambao walistaafu kwa sababu yeyote ile hawarusiwi kuomba.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **10/08/2022** saa **9:30** alasiri.

Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi,
S.L.P 70,
ITIGI.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:



John K. Mgalula

MKURUGENZI MTENDAJI (W)



Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022.

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI**

Nakala: Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320,
DODOMA.

- Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi www.itigidc.go.tz
- Mbao za Matangazo